## Suala kuu la 4

## Mvua ya kutwa

'Hauchi hauchi unakucha!' Denzel aliwazia msemo huo ambao sasa ulikuwa umepata maana. Hatimaye, siku aliyoisubiri kwa hamu na hamumu ilikuwa imewadia.

Alasiri ya siku hiyo, mjomba wake, Bwana Mambo, angeasi ukapera katika sherehe ya harusi, kisiwani Lamu. Wazazi wa Denzel walikuwa wameahidi kwamba wangeandamana na Denzel kwenda kuhudhuria harusi ile. Denzel alifurahi sana kwani hakuwa amewahi kufika Lamu.

"Ni furaha iliyoje kusafiria mashua kwa mara ya kwanza maishani?" Denzel alijisemea.

Denzel aliamka alfajiri, mwendo wa saa kumi na moja kasorobo, ili kujiandaa. Baada ya kusali, aliingia bafuni kuoga. Saa kumi na moja na nusu, alikuwa ameshapata kiamshakinywa. Saa thenashara kamili asubuhi, alipiga mswaki kisha akavaa suti yake mpya iliyomkaa vizuri. Walipokuwa tayari kuondoka, saa kumi na mbili na nusu, mvua ilianza kunyesha! Ilinyesha kwa muda wa dakika arubaini na tano bila kupusa.

Denzel alishikwa na wasiwasi kama mwasi. Wazazi wake pia waliingiwa na hofu. Waliketi sebuleni wakingoja mvua ipuse huku wakitazama taarifa kwenye runinga. Kadiri muda ulivyozidi kusonga, ndivyo mvua ilivyozidi kuongezeka! Ingepusa kwa dakika tano na kuongezeka tena. Habari iliyosomwa kwenye runinga ilipotimia saa tano kamili, ndiyo iliyowavunja moyo zaidi.

"Mvua kubwa inayoendelea kunyesha maeneo ya Pwani imetatiza shughuli nyingi za wakazi. Wizara ya usalama imetoa tahadhari kwa wakazi wawe waangalifu, ikisema kuwa mvua hiyo inatarajiwa kuendelea mchana wote. Barabara nyingi za maeneo ya Pwani tayari hazipitiki! Aidha, wananchi wameshauriwa wasitishe shughuli zote baharini zikiwemo usafiri na uogeleaji," alihitimisha mtangazaji.

Mambo yalikuwa vilevile hata ilipotimia saa saba mchana. Ilikuwa dhahiri safari ilikuwa imetumbukia nyongo. Denzel na wazazi wake, hata hivyo, hawakuwa na habari kama harusi ya Bwana na Bi. Mambo ilifanyika au la. Mvua ile ilikatika machweo, wakati maji yalikuwa yamemwagika na yasingezoleka. Denzel asingeweza kuisahau siku ile.